



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

*Barua zote zianjikwe na kutumwa kwa:*

Simu: +255 262 965 732 (Direct line)

Nukushi: +255262965732

Barua Pepe: [ded@sikongedc.go.tz](mailto:ded@sikongedc.go.tz)

Tovuti: [www.sikongedc.go.tz](http://www.sikongedc.go.tz)

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilayaya Sikonge,  
4 MTAA WA BOMANI,  
S.L.P 70,  
45382 SIKONGE-TABORA

Tarehe: 30.01.2023

## TANGAZO

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge anapenda kuwatangazia Wananchi wote Wilaya ya Sikonge kuweza kuomba nafasi ya kuwa Mjumbe katika Kamati ya Usimamizi na uendeshaji wa Huduma za Afya (**Health Facility Governing Committee**) katika Hospitali ya Wilaya ya Sikonge kwa kipindi cha Miaka Mitatu.

### NAFASI ZINAZOTANGAZWA:-

1. Wawakilishi wa Watumiaji wa Huduma za Hospitali – **Nafasi 03**
2. Mjumbe kutoka Huduma za Afya Binafsi - **Nafasi 01**
3. Mjumbe kutoka Huduma za Afya za Taasisi/Asasi za Jamii (FBO's/NGO's) – **Nafasi 01**

### SIFA ZA WAOMBAJI:-

Sifa za waombaji wa Kamati ya usimamizi na uendeshaji wa Huduma za Afya Hospitali ya Wilaya ya Sikonge (HFGC) wanahitajika kuzingatia vigezo vifuatavyo wakati wa kutuma Maombi:-

#### 1. UMRI

o Kwa kuzingatia kazi za Kamati, umri unaopendekezwa utakuwa kati ya miaka 21 na kuendelea. Hivyo muombaji aambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa katika barua ya Maombi.

#### 2. URAIA

o Wajumbe wanaowakilisha watumiaji wa huduma na Kamati za usimamizi za Hospitali za vituo vya Serikali watakuwa raia wa Tanzania, lakini hii haitakuwa lazima kwa wajumbe kutoka Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

#### 3. ELIMU

o Waombaji wanatakiwa kuwa wamehitimu kuanzia Elimu ya Sekondari na kuendelea.

#### 4.SIFA NA VIGEZO VINGINEVYO VYA KUZINGATIA

- Awe Mwanachama hai wa Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii itiyoboreshwa (ICHF)
- Awe na uelewa namna ambavyo shughuli mbalimbali za Idara ya Afya zinavyotekelezwa katika ngazi ya Halmashauri
- Asiwe amewahi kutwa na kosa lolote la Jinai katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Awe ni Mkazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge
- Asiwe na wadhifa wowote wa kisiasa kupitia chama chochote cha Siasa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Asiwe Mwajiriwa wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ama Muajiriwa wa Halmashauri husika
- Maombi yote yaambatane na Risiti ya Malipo ya Fedha taslimu ,kiasi cha TZS 10,000/= inayotakiwa kulipwa katika akaunti ifuatayo;NMB 51210013092 Hospitali ya Wilaya ya Sikonge.Fedha haitarudishwa endapo Mjumbe hata pata nafasi ya kuchaguliwa

Maombi yote yatumiwe kwenda kwa

Mkurugenzi Mtendaji (W).

S.L.P 70.

SIKONGE

Mwisho wa kutuma maombi ni Ijumaa tarehe 28.02.2023 saa saba kamili (7.00 Mchana.)

Imetolewa na:

  
Nico Kayarige

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)

SIKONGE.

MPURUNGUZI MTENDAJI  
WILAYA SIKONGE